



CSD & REGISTRY COMPANY LIMITED

TANGAZO

KUSITISHA UTOAJI WA RISITI YA UWEKAJI

Tunapenda kuwafahamisha Mawakala wa Soko la Hisa la Dar es salaam (DSE), Benki zinazotunza dhamana za wawekezaji, Kampuni za uwekezaji, Taasisi za Fedha, Wawekezaji na Wananchi kwa ujumla kuwa, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) imepitisha Kanuni mpya za Soko la Hisa na Hifadhi ya Dhamana (DSE – CSD Rules 2022). Hivyo kuanzia tarehe **1 Aprili 2022**, CSDR itasitisha utoaji wa **Risiti ya Uwekezaji (Depository Receipt)** maarufu kama Cheti cha Hisa kwa hisa zote zitakazonunuliwa kwenye Soko la Pili (yaani DSE).

Badala ya Risiti ya Uwekezaji (Depository Receipt), CSDR itatoa **Taarifa ya Akaunti** kama uthibitisho wa umiliki wa dhamana kwa mwekezaji. Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 5(1) inayosema **“Taarifa ya Akaunti inayotolewa na CSDR itakuwa ndiyo uthibitisho wa umiliki wa dhamana husika”**

CSDR itaendelea kutuma Taarifa ya Akaunti moja kwa moja kwa wanahisa kwa barua pepe kila mwisho wa mwezi. CSDR inatoa wito kwa Wanahisa wote kuwasiliana na Mawakala wa Soko la Hisa ili kuhuisha taarifa zao za mawasiliano ikiwemo anuani, namba ya simu na barua pepe ili kuwezesha utumaji wa Taarifa za Akaunti.

Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na:

Mkurugenzi Mkuu,
CSD & Registry Company Limited (CSDR),
Mtaa wa Ufukoni, Jengo la Kambarage, Ghorofa ya Pili,
S. L. P 70081,

DAR ES SALAAM

Simu: 0746 160516 / 0677 070414

Barua pepe: info@csdr.co.tz